

## Maelezo ya Ukweli Kuhusu COVID-19

### Kuelewa jinsi chanjo tofauti za COVID-19 zinavyofanya kazi

Chanjo ya COVID-19 inaweza kuwasaidia watu kupata kinga dhidi ya SARS-CoV-2, ambavyo ndivyo virusi vinavyosababisha COVID-19, bila kuugua. Chanjo tatu zimeidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya dharura nchini Marekani na zinapatikana kwa wakazi wa Ohio wanaostahiki kupipokea. Chanjo hizi tofauti za COVID-19 zinafanya kazi kwa namna gani hasa? Zinafanana vipi? Zinatofautiana vipi? Zote ni [salama na zenye ufanisi](#)? Haya ndiyo mambo unayopaswa kujua kuhusu chanjo hizi.

#### ***Chanjo za COVID-19: Muhtasari wa Maelezo ya Ukweli***

	<b><i>Pfizer-BioNTech</i></b>	<b><i>Moderna</i></b>	<b><i>Johnson &amp; Johnson (Janssen)</i></b>
<b><i>Tarehe ya kuidhinishwa</i></b>	Desemba 11, 2020	Desemba 18, 2020	Februari 27, 2021
<b><i>Aina ya chanjo</i></b>	<a href="#">Messenger RNA (mRNA)</a>	<a href="#">Messenger RNA (mRNA)</a>	<a href="#">Chanjo za kuwasilisha chembejeni katika seli</a>
<b><i>Dozi</i></b>	Dozi mbili, siku 21 kati ya dozi ya kwanza na ya pili	Dozi mbili, siku 28 kati ya dozi ya kwanza na ya pili	Dozi moja
<b><i>Umri</i></b>	16 na zaidi	18 na zaidi	18 na zaidi
<b><i>Data za ufaafu wa chanjo kutokana na majaribio ya kimatibabu</i></b>	Uwezo wa asilimia 95 wa kuzuia visa vya COVID-19 vilivyothibitishwa katika maabara, kwa watu waliopokea dozi mbili za chanjo.	Uwezo wa asilimia 94 wa kuzuia visa vya COVID-19 vilivyothibitishwa katika maabara, kwa watu waliopokea dozi mbili za chanjo.	Kinga kamili dhidi ya kulazwa hospitalini, na mauti yanayotokana na ugonjwa wa COVID-19, ufanisi wa asilimia 85 katika kuzuia kudhurika vikali na COVID-19, na ufanisi wa asilimia 72 nchini Marekani (asilimia 66 kwa jumla) katika kuzuia visa vya wastani hadi vibaya vya COVID-19.
<b><i>Athari za chanjo</i></b>	Maumivu kwenye eneo lililodungwa, uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, maumivu ya maungo, homa. Mara nyingi athari hizi hushuhudiwa baada ya dozi ya pili. Ni nadra kushuhudia mizio mikali.	Maumivu kwenye eneo lililodungwa, uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, maumivu ya maungo, homa. Mara nyingi athari hizi hushuhudiwa baada ya dozi ya pili. Ni nadra kushuhudia mizio mikali.	Maumivu kwenye eneo lililodungwa, maumivu ya kichwa, uchovu, na maumivu ya misuli. Sio watu wengi waliopata kichefuchefu na homa. Chanjo hii haijahusishwa na visa vya kushuhudia mizio mikali baada ya kuipokea.
<b><i>Hati za Maelezo ya Ukweli</i></b>	<a href="#">Maelezo ya Ukweli Kuhusu Idhini ya Matumizi ya Dharura ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech</a>	<a href="#">Maelezo ya Ukweli Kuhusu Idhini ya Matumizi ya Dharura ya Chanjo ya Moderna</a>	<a href="#">Maelezo ya Ukweli Kuhusu Idhini ya Matumizi ya Dharura ya Chanjo ya Janssen</a>

#### ***Chanjo zitasambazwa vipi katika jimbo la Ohio?***

Huku bado kukiendelea kuwapa uhaba wa chanjo, watu wanaopokea chanjo za COVID-19 huenda wasipewe nafasi ya kuchagua aina ya chanjo wanayotaka kupewa.

Chanjo inayopatikana katika kituo fulani cha kutoa chanjo au kliniki ndiyo chanjo ambayo mtu atapokea. Kupewa chanjo kwa kutumia chanjo ya kwanza unayoweza kupata kunaweza kukusaidia kujikinga dhidi ya COVID-19.

Imethibitishwa kwamba chanjo zote tatu za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi katika kuzuia maradhi makali, kulazwa hospitalini, na mauti yanayotokana na ugonjwa wa COVID-19.

## **Aina tofauti za chanjo**

Chanjo ndizo kinga thabiti zaidi katika kuzuia kudhurika vikali na COVID-19. Chanjo hukupa kinga ili mwili wako ukumbuke jinsi ya kupambana na virusi katika siku zijazo.

Chanjo za COVID-19 za nchi ya Marekani hufanya kazi kwa namna tofauti, lakini zote zinahusisha matumizi ya protini za utando wa virusi vya SARS-CoV-2, ambavyo husababisha COVID-19, ili kujenga kinga.

Protini za utando hugandisha virusi hivyo kwenye seli, ili kuruhusu virusi kupenyeza ndani ya seli hizo. Protini ya utando haina madhara, na kuitumia katika chanjo huufunza mwili wako tu kuhusu jinsi ya kutambua protini hiyo, na jinsi ya kupambana nayo katika siku zijazo.

## **Chanjo za Messenger RNA (mRNA)**

[Chanjo za Messenger RNA \(mRNA\)](#) hutumia mikanda ya kijeni inayoitwa [mRNA](#) ili kuwasilisha msimbo wa kijeni kwenye seli ili kutengeneza utando au protini kwenye virusi vya SARS-CoV-2. Protini zilizotengenezwa kwa maelekezo ya mRNA huuwasha mfumo wa kinga, kuufunza kutambua protini ya utando kama adui, na kubuni kingamwili za kupambana nayo. Mwili hujifunza jinsi ya kujikinga kutokana na maambukizi yanayoweza kutokea baadaye.

Teknolojia hii ya chanjo hutumika katika [chanjo za](#) Pfizer-BioNTech [na](#) Moderna. Hata ingawa chanjo za mRNA hazijakuwepo kwa muda mrefu, watafiti wamekuwa wakitafti na kutumia chanjo za mRNA kwa miongo mingi. Hapo awali, zimefanyiwa utafiti kwa ajili ya maradhi kama vile mafua, homa ya Zika, na kichaa cha mbwa. Mbali na chanjo, utafiti wa ugonjwa wa saratani umetumia mRNA ili kuchochea mfumo wa kinga kulenga seli mahususi zenye saratani.

## **Chanjo za kuwasilisha chembejeni katika seli**

Chanjo [ya kuwasilisha chembejeni katika seli](#) hutumia muundo uliobadilishwa wa virusi tofauti ili kuwasilisha maagizo kwa seli na kurudufu protini za utando. Virusi visivyo hai na visivyo na madhara, kama vile vinavyosababisha mafua, hutumika kama kisafirishaji cha kuwasilisha maagizo ya kutengeneza protini ya utando. Mfumo wa kinga kisha hutambua kwamba protini hii haipo mahali sahihi, ndipo sasa unaanza kupambana nayo. Mwili hujifunza jinsi ya kujikinga kutokana na maambukizi yanayoweza kutokea baadaye.

Teknolojia hii hutumika katika [chanjo ya Johnson & Johnson \(Janssen\)](#). Wanasayansi walianza kutengeneza chanjo za kuwasilisha chembejeni katika seli katika miaka ya 1970. Kando na kutumika kama chanjo za magonjwa kama mafua na virusi vya RSV, chanjo za kuwasilisha chembejeni katika seli pia zimefanyiwa utafiti wa kutoa matibabu ya kijeni, kutibu saratani, na kwa utafiti wa biolojia ya molekulya. Chanjo zinazotumia teknolojia hii zilitumika wakati wa mlipuko wa Ebola.

## **Chanjo hubainishwa vipi kwamba ni salama na zenye uwezo wa kukupa kinga?**

Usalama wa chanjo za COVID-19 unachunguzwa kwa makini na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) pamoja na mamlaka ya Marekani ya Usimamizi wa Chakula na Dawa (FDA).

Mamlaka ya FDA inaweza kutoa [idhini ya matumizi ya dharura](#) (EUA) ili kuhakikisha bidhaa za matibabu zinapatikana kwa haraka wakati wa visa vya hatari kwa ajili ya usalama wa umma kama vile janga la COVID-19. Mamlaka ya FDA hutumia viwango vya juu na ushauri kutoka kwa wataalamu huru wa matibabu ili kutathmini data zote zilizopo na kuhakikisha kwamba chanjo ni salama na faafu, na kwamba manufaa ya matumizi yake yanazidi hatari zozote zinazoweza kutokana na kutumia chanjo hiyo. Baada ya FDA kutoa maamuzi, shirika la CDC pia hupitia data zilizopo kabla ya kutoa mapendekezo ya mwisho kuhusu matumizi ya chanjo. [Mifumo ya kufuatilia usalama wa chanjo](#) huendelea kufanya kazi baada ya chanjo kuanza kutumika.

### **Nyenzo:**

- [Idhini ya Matumizi ya Dharura ya Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech](#)
- [Idhini ya Matumizi ya Dharura ya Chanjo ya COVID-19 ya Moderna](#)
- [Idhini ya Matumizi ya Dharura ya Chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson \(Janssen\).](#)

## **Kuelewa ufaafu wa chanjo kupitia majaribio ya**

Pengine huenda umesikia kuhusu viwango vya ufaafu wa chanjo za COVID-19. Lakini nambari hizi zinamaanisha nini hasa? [Ufaafu wa chanjo](#) ni asilimia ya kiwango cha ugonjwa kinachopungua katika kundi la watu ambao wamepokea chanjo katika majaribio yake ikilinganishwa na washiriki wa majaribio hayo ambao hawakupokea chanjo hiyo. Kwa mfano, ufaafu wa kiwango cha asilimia 85 unamaanisha kwamba watu waliopokea chanjo walikuwa na hatari ya chini ya kudhurika na COVID-19 kwa asilimia 85 ukilinganisha na washiriki ambao hawakupata chanjo.

Kulinganisha ufaafu wa hizi chanjo tatu za COVID-19 kuna changamoto kwa sababu ya tofauti zilizopo katika miundo na nyakati za utekelezaji wa Awamu ya 3 ya majaribio ya chanjo hizo. Majaribio hayo yalikuwa yanachunguza uwezekano wa kuibuka kwa matokeo tofauti, chanjo hizo hazikulinganishwa moja dhidi ya nyingine, na zote hazikutumika kuchunguza ufaafu wake dhidi ya [virusi vipya vilivyobuka](#). Ulinganisho huu hauangazii mambo yaliyo sawa.

- Majaribio ya chanjo za [Pfizer](#) na [Moderna](#) yalifanyika ili kubaini ikiwa chanjo hizo zilizuia maambukizi yoyote ya COVID-19 ambapo mgonjwa anaonyesha dalili za ugonjwa huo.
- [Majaribio ya chanjo ya Janssen](#) yalitekelezwa ili kubaini ikiwa chanjo hiyo ilimzuia mtu kudhurika kwa COVID-19 kwa kiwango cha wastani au cha juu, kwa msingi wa matokeo ili kuonyesha kwamba ana virusi hivyo na mgonjwa ana angalau dalili moja ya ugonjwa huo.
- Chanjo za Pfizer na Moderna zilifanyiwa majaribio karibu wakati sawa kabla [ya kuibuka kwa virusi vipya](#) nchini Uingereza, Afrika Kusini na Brazil. Bado haijulikana vipi chanjo hizi zitaweza kupambana na virusi hivi vinavyobadilika, ingawa utafiti wa mapema unaonyesha kwamba chanjo hizi bado zinawapa watu kinga. Chanjo ya J&J ilifanyiwa majaribio baadaye wakati virusi vipya vilikuwa vinaibuka, na visa vya jumla vya maaambukizi vilikuwa juu zaidi.

La msingi ni kwamba chanjo zote tatu zinakuinga dhidi ya maradhi makali, ikijumuisha kulazwa hospitalini na mauti.

*Iliundwa mnamo Februari 28, 2021.*

Kwa maelezo ya ziada, tembelea [coronavirus.ohio.gov](https://coronavirus.ohio.gov). Ili kupata majibu ya maswali yako kuhusu COVID-19, piga simu kupitia 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634) au utume barua pepe kwenda [COVIDVACCINE@odh.ohio.gov](mailto:COVIDVACCINE@odh.ohio.gov).

**Afya ya akili yako ni muhimu kama ilivyo afya ya mwili wako. Ikiwa wewe au mpendwa wako anashuhudia wasiwasi unaohusiana na janga la COVID-19, kuna usaidizi unaopatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Piga simu kwa huduma ya usaidizi unaohusiana na COVID-19 kupitia 1-800-720-9616.**